# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NNE

**03 NOVEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 03 NOVEMBA, 2023

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**45. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani kuruhusu Kata za Kanindo, Igombemkulu na Milambo kufanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Udiwani.

**46. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Kifura - Muhambwe.

**47. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Walimu kukidhi mahitaji katika Shule za Sekondari na Msingi Wilayani Namtumbo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**48. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ipo tayari kuleta marekebisho ya Sheria baada ya Serikali kukubaliana kuondoa baadhi ya changamoto za Muungano.

## WIZARA YA KILIMO:

**49. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa nini Wakulima wa Kahawa Mbozi wanakatwa Shilingi 200 kwa kilo licha ya tamko la kusitisha tozo hiyo.

**50. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Kihungu - Mbinga.

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**51. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA KISAU (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Mnara wa Mawasiliano wa TBC – Kiteto.

**WIZARA YA UJENZI:**

**52. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Katumba - Mbambo - Tukuyu utasainiwa kwa kuwa Mkandarasi alishapatikana.

**53. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kwa nini Serikali isitumie teknolojia na vifaa vya kisasa kusafisha barabara za *TANROADS.*

**54. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini *TANROADS* watalipa fidia kwa kujenga shule mbadala baada ya Shule ya Msingi Unkuku kupitiwa na Barabara ya Dodoma – Arusha.

**55. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Lami kutoka Kawajense – Ugalla hadi Kahama.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**56. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itabadili Mitaala ya Elimu ili kwenda na wakati.

**57. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini Ukumbi wa VETA Nyasa haujawekwa vipooza joto.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**58. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuifanya Bandari ya Tanga iwe na ufanisi zaidi.

**59. MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (KILOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakarabati na kufufua reli kutoka Kilosa hadi Kidatu.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**60. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Wazee zaidi ya miaka 60 wanaostahili kupata huduma za afya bila malipo wanapata huduma hizo.

**WIZARA YA AFYA:**

**61. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali haioni kuna haja ya Watoto wachanga kutumia Bima za Afya za Mama zao.

**WIZARA YA MAJI:**

**62. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka mradi wa maji katika Kata za Kizumbi na Wampembe - Nkasi Kusini.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**63. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Mahakama ya Wilaya Urambo.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**64. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Taifa linanufaika kiasi gani katika uuzaji wa bidhaa na huduma katika maeneo ambayo Jeshi letu linafanya ulinzi wa amani.

**WIZARA YA NISHATI:**

**65. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mkoa wa Rukwa utaunganishwa na Gridi ya Taifa ya umeme.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**66. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Jeshi la Wananchi litatimiza ahadi yake ya kujenga daraja la dharula katika Mto Mtitu Kata ya Ihimbo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**67. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa utambuzi wa Mifugo baada ya kusitisha zoezi la utambuzi kwa kutumia hereni za mifugo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**68. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKSHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Sheria ipi inawaruhusu Watumishi wa TANAPA, TAWA na NCAA kutoza Mifugo Shilingi 100,000/= pindi iingiapo Hifadhini.

## III. HOJA ZA KAMATI:

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **03 NOVEMBA, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |